KONZA
Technopolis

Ruwaza

Kuwa jiji teknolojia la kimataifa na kitovu cha uvumbuzi ulimwenguni

Azma kuu

Kujenga jiji endelevu la kiteknolojia linalonawiri na kuendeleza uvumbuzi unaochangia ukuaji wa uchumi wa kimaarifa Kenya

Mkataba wa Utoaji wa Huduma

Maadili Makuu

Ukuzaji	Tunatambua na kuwekeza katika ukuzaji wa vipaji na taaluma mbalimbali ili kuafikia ruwaza yetu. Tunaona nafasi za ukuzaji mbele yetu huku tukijizatiti kuafikia upeo wa jiji la kiteknolojia la Konza.
Uvumbuzi	Twachagua kubadilisha na kuboresha hali katika chochote tunachofanya. Tuna hamu ya kujua, ubunifu na hamasa ya kutafuta mbinu bora zaidi za kuwasilisha bidhaa na huduma kwa wateja wetu.
Ushirikiano	Tunaafikia malengo mengi kwa kufanya kazi kwa pamoja. Tunaongeza mchango wetu kupitia mikakati ya ushirikiano inayofaidi wadau wetu wote.
Uweledi	Tuna azma ya kuwasilisha jiji la kiteknolojia la Konza lenye ubora wa kuishi, kufanya kazi, na kucheza kupitia mbinu za kipekee zinazowasilisha huduma kwa wakati ufaao. Twafanya biashara yetu kwa uadilifu kwa njia ya uwazi, uwajibikaji na maadili mema.

Huduma	Ahadi Yetu	Muda	Ada	Matarajio kutoka wadau wetu
Majibu kuhusu maswali ya wateja na mawasiliano na mahitaji mengine ya maelezo	Kuwahudumia wageni	Ndani ya dakika tano (5)	Bila malipo	Tembelea afisi za KoTDA Kuhudhuria mikutano ya KoTDA unapoalikwa na kuheshimu mwaliko wa mikutano na wakati kama ilivyopangwa Kuonyesha heshima na staha kwa wafanyakazi wa KoTDA Kujifahamisha na sheria, kanuni na masharti mengine ya kisheria, ambayo huongoza shughuli za KoTDA
	Kupokea simu	Ndani ya sekunde tano (5) sawa na muda wa simu kuita mara tatu (3)	Bila malipo	Kupiga simu kwa kutumia nambari za simu zilizotolewa
	Kujibu maswali: a) Barua pepe b) Mitandao ya kijamii	Katika kipindi cha siku saba (7) Katika kipindi cha siku mbili (2)	Bila malipo Bila malipo	Wasilisha maombi ya maelezo na habari kupitia anwani rasmi za barua pepe na mitandao ya kijamii
	Barua ya Posta/tarishi/kuwasilisha mwenyewe a) Mawasiliano ya kawaida b) Kiufundi	Ndani ya siku saba (7) Ndani ya siku ishirini na moja (21)	Bila malipo Bila malipo	Ombi la maelezo au habari kwa maandishi
Usaidizi kwa Wawekezaji	Kusajili kwa wawekezaji	Ndani ya siku thelathini (30)	Bila malipo	Jaza fomu ya KoTDA inayopatikana mtandaoni. Ambatisha nyaraka muhimu zinazohitajika
	Kutoa MoU/NDA	Ndani ya siku kumi (10)	Bila malipo	Kutoa habari na ushirikiano au ubia
	Kufanikisha ziara za kutembelea eneo	Ndani ya siku tano (5)	Bila malipo	Wasilisha ombi rasmi
	Kutoa idhinisho	Ndani ya siku sitini (60) rasmi za kazi	Bila malipo	Wasilisha maombi yaliyohakikiwa & nyaraka zifaazo kwa Kamati ya Utathmini, ndani ya siku 30 za kazi, na kwa Bodi ya KoTDA ndani ya siku thelathini (30) za kazi
Malipo ya bidhaa na huduma	Kamilisha malipo kwa bidhaa zilizowasilishwa na huduma zilizotolewa kwa mujibu wa makubaliano	Ndani ya siku thelathini (30) rasmi za kazi baada ya kupokea ombi la kudai malipo, au kwa mujibu wa mkataba	Bila malipo	Wasilisha dai la malipo/ombi la malipo Wasilisha bidhaa na kutoa huduma za ubora kuambatana na makubaliano
	Kutoa risiti	Ndani ya siku moja (1) ya kufanya kazi	Bila malipo	Fanya malipo
Ununuzi wa bidhaa na huduma	Fuata na kuheshimu sheria na kanuni za ununuzi wa bidhaa na huduma	Kila wakati	Bila malipo	Wasilisha bidhaa na kutoa huduma za ubora wa hali ya juu / Fuata na kuheshimu sheria na kanuni za ununuzi wa bidhaa na huduma
Huduma za mtandao	Dumisha mtandao ulio rahisi kutumia na wenye maelezo na habari sahihi	Kila wakati	Bila malipo	Mara kwa mara tembelea tovuti ya KoTDA na kuwasilisha maombi ya taarifa na/au maoni ifaavyo

Haki Za Mteja

Haki ya kupata habari

Ni haki yako kupata habari na maelezo kamili, sahihi na kwa wakati kuhusu vitendo na wajibu wako chini ya Sheria mbalimbali.

Haki ya kutokosoa

Ni haki yako kukosoa habari na maelezo, ushauri au huduma tunayotoa kwako. Tutakufahamisha kuhusu njia mbalimbali zinazoweza kutumiwa kutatua migogoro na tutashirikiana nawe kupata suluhu ya haraka na kwa njia rahisi.

Kujitambulisha

Ni haki yako kuitisha kitambulisho rasmi cha kazi cha KoTDA kutoka kwa wafanyakazi wowote wetu watakaokutembelea au wanaokuhudumia katika nafasi rasmi. Ukiwa na shaka, unaweza kuwasiliana na KoTDA kuthibitisha utambulisho wa afisa yeyote yule.

Heshima na kuzingatiwa

Una haki ya kushughulikiq kwa heshima, kwa njia ya kujali na isiyobagua katika shughuli zozote zile na maafisa wa KoTDA iwe ni wakati wa kutaka habari na maelezo, kupanga mikutano au shughuli nyingine yoyote ile inayohusiana na KoTDA.

Kuwa mkweli

Unaaminika kuwa mkweli na mwenye uwazi, isipokuwa tu pale kunapokuwa na ushahidi wa kuthibitisha kinyume.

Usiri na faragha

Unahakikishiwa kwamba taarifa na maelezo yako binafsi na ya kifedha ambazo unatoa kwa KoTDA vyote vitatumiwa tu kwa madhumuni ya kutekeleza shughuli zinazokubalika kisheria, ila tu pale tutakapokuwa na idhini yako ya kuvitumia kwa njia nyingine au katika hali nyingine zinazokubalika kisheria.

Upatikanaji wa Habari

Afisa Mkuu Mtendaji
Mamlaka ya Ustawi wa Konza Technopolis

Orofa ya 7, jumba la Konza Complex, Nairobi – Mombasa road – Konza

Sanduku la posta 1 – 90150 Konza Technopolis

+254(0) 204343013/4
konza@konza.go.ke, ceo@konza.go.ke

www.konza.go.ke

Konza Technopolis @konzatech

Malalamishi

Afisa Mkuu Mtendaji
Mamlaka ya Ustawi wa Konza Technopolis

Orofa ya 7, jumba la Konza Complex, Nairobi – Mombasa road – Konza

Sanduku la posta 1 – 90150 Konza Technopolis

+254(0) 204343013/4
konza@konza.go.ke, ceo@konza.go.ke

www.konza.go.ke

complaints@konza.go.ke

Afisi ya Tume ya Malalamishi ya Umma (Afisi ya Ombudsman)

Orofa ya 2, Jumba la West End Towers, Mkabala na Shule ya Aga Khan High, Barabara ya Waiyaki – Westlands

S.L.P 20414 – 00200 Nairobi
Simu : +254-20-2270000 /2303000
/ 2603765 / 2441211 / 8030666

info@ombudsman.go.ke - kwa habari na maelezo
complain@ombudsman.go.ke - kwa malalamiko.